

## SEKTA YA AFYA

Wakala wa Vipimo inafanya uhakiki wa mizani zinazotumika kwenye vituo vya afya ili kutoa uzito sahihi wa wagonjwa na watoto mara wanapozaliwa.



Uhakiki wa mizani kwenye sekta ya Afya

## SEKTA YA USAFIRISHAJI (BARABARA, MAJINI NA ANGANI)

Wakala wa Vipimo inahakiki Mizani zinazotumika kupimia uzito wa magari yapitayo kwenye Barabara kwa lengo la kulinda miundombinu ambayo imejengwa na serikali isiharibike mapema. Kadhalika, uhakiki unafanyika kwenye mizani inayotumiwa kwenye usafiri wa anga na usafiri wa majini pamoja na kuhakiki vipimo vya ujazo vinavyotumika kwenye sekta ya usafirishaji.



Uhakiki wa mizani ya Barabarani



### KWA MAWASILIANO ZAIDI:

Afisa Mtendaji Mkuu,  
Wakala wa Vipimo, Mtaa wa Uhuru,  
Vipimo House, S.L.P 2014, Medeli,  
Dodoma, Tanzania.

Simu: +255 262 610 700

Namba ya Bure: 0800 110097

Barua pepe: [info@wma.go.tz](mailto:info@wma.go.tz)

Tovuti: [www.wma.go.tz](http://www.wma.go.tz)

Instagram: [wakalawavipimotanzania](https://www.instagram.com/wakalawavipimotanzania)



## WAKALA WA VIPIMO (WMA)

Wakala wa Vipimo (WMA) ni mojawapo ya Wakala za Serikali ambayo ilianzishwa tarehe 13 Mei, 2002 kwa Tangazo la Serikali namba 194 la tarehe 17 Mei, 2002 na inatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria ya Vipimo Sura Na. 340. Awali, ilikua ni Idara chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara.

## MAJUKUMU YA WAKALA WA VIPIMO

Wakala wa Vipimo inalo jukumu la kumlinda mlaji na umma kwa ujumla kupitia uhakiki na uthibiti wa vipimo vinavyotumika katika biashara na huduma nyingine, kuhakikisha kuwa vipimo hivyo ni sahihi na vinatumika kwa usahihi kulingana na Sheria ya Vipimo Sura 340 mapitio ya mwaka 2002 na maboresho yake ya mwaka 2016 pamoja na kanuni zake.

## SEKTA YA BIASHARA

Wakala wa Vipimo inafanya uhakiki wa vipimo katika maeneo mbalimbali ya biashara kama maduka ya kuuzia nyama, Viwandani, mizani inayotumika kuuzia bidhaa masokoni ikiwemo bidhaa zilizofungashwa ili kuhakikisha wananchi wanapata bidhaa kwa usahihi kulingana na thamani ya fedha inayotolewa.



Maafisa Vipimo wakifanya uhakiki wa bidhaa zilizofungashwa



## SEKTA YA KILIMO

Wakala wa vipimo inafanya uhakiki wa mizani zote zinazotumika wakati wa ununuzi wa mazao mbalimbali kama zao la pamba, korosho na ufuta. Uhakiki huo wa mizani ya vyama vya msingi vya ushirika na makampuni yanayo nunua mazao hufanyika kabla ya msimu kuanza na usimamizi mara baada ya msimu kuanza ili kujiridhisha kama inatumika kwa usahihi.



Uhakiki wa mizani inayotumika kununulia zao la pamba na Korosho

## SEKTA YA MAJI

Wakala wa vipimo inafanya uhakiki wa mizani zote zinazotumika wakati wa ununuzi wa mazao mbalimbali kama zao la pamba, korosho na ufuta. Uhakiki huo wa mizani ya vyama vya msingi vya ushirika na makampuni yanayo nunua mazao hufanyika kabla ya msimu kuanza na usimamizi mara baada ya msimu kuanza ili kujiridhisha kama inatumika kwa usahihi.



Uhakiki wa Dira za Maji

Benchi inayotumika kupima dira za maji



## SEKTA YA MADINI

Wakala wa Vipimo inahakiki mizani zinazotumika kununulia madini na vito vya thamani na migodini, katika masoko ya kuuzia madini na kwa wauzaji wa madini (sonara). Pia, tunatoa ushauri wa kitaalamu kwa Wizara inayohusika na madini mara kwa mara inapohitajika.



Dhahabu ikipimwa kwenye mizani uliohakikiwa

## SEKTA YA MAFUTA

Wakala wa Vipimo inafanya uhakiki katika sekta ya mafuta tangu yanapoingia nchini kwa njia ya meli ili kuhakiki kiasi cha mafuta yaliyoingia nchini, Uhakiki wa flow meters za bandarini zinazopima mafuta kutoka kwenye maghala, uhakiki wa matenki makubwa ya kuhifadha mafuta ( bulk storage tanks), Uhakiki wa matenki ya malori yanayotumika kusafirishia mafuta, uhakiki wa matenki makubwa yaliyo chini ya ardhi yanayotumika kuhifadhi mafuta pamoja na uhakiki wa pampu zote za kuuzia mafuta.



Uhakiki wa pampu za kuuzia mafuta



Uhakiki wa matenki ya malori yabebayo mafuta